


HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Arusha,
Telegram: Arusha.
Simu: 073 6500476,
Faksi: 250 3701.
Email: ded@arushadistrict.go.tz

www.arushadc.go.tz



Ukumbi wa Wilaya,
S. L. P. 2330,
ARUSHA.

MIRADI YA TASAF AWAMU YA III INAYOTEKELEZWA KATIKA HALMASHAURI YA ARUSHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

UTANGULIZI.

Mpango wa TASAF (Tanzania Social Action Fund) ulianza mwaka 2000 ukiwa na lengo la kukabiliana na athari za mtokeo ya mabadiliko ya kiuchumi katika miaka ya 1990 yaliyosababisha kuwepo na mahitaji makubwa katika huduma za msingi.

Ingawa ilionekana kiwango cha umaskini kupungua lakini jamii kubwa ilikuwa inaishi katika umaskini uliokithiri kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukame, kushuka kwa bei ya mazao ya biashara, kupanda kwa bei za mazao ya chakula, maradhi na vifo.

Hali hii ilipelekea kuwepo kwa mpango maalum wa kupambana na umaskini. Lengo kuu la mpango wa kupambana na umasikini ni kuwezesha jamii kuboresha maisha kwa kupata huduma bora.

Nchini Tanzania mpango wa TASAF umetekelezwa katika awamu tatu tofauti yaani TASAF awamu ya I ilitekelezwa mwaka 2000-2005, TASAF awamu ya II ilitekelezwa mwaka 2005-2013. Halmashauri ya Arusha haikutekeza mradi wowote katika awamu ya kwanza TASAF.

Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ni miongoni mwa Halmashauri zilizofanikiwa kutekeleza mpango wa TASAF awamu ya II na ya III. Utekelezaji unalenga kuboresha sekta za umma kwa njia ya ujenzi wa miundombinuu ya elimu, afya, mawasiliano na kilimo.

TASAF awamu ya II 2005-2013:

Halmashauri ya Wilaya ya Arusha Ilianza kutekeleza mpango wa TASAF awamu ya II kuanzia mwaka 2005-2013 ikiwa ni moja ya njia ya utekelezaji wa MKUKUTA (Mpango wa Kupunguza na Kuondoa Umaskini Tanzania) na Malengo ya Milenia (Millennia Development Goals). Ililenga kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya, elimu, uchumi, kilimo, maji, kusaidia makundi maalum (yatima, wajane, wanaoishi na vvu/ukimwi) kwa kuzingatia

MKUKUTA na MDGs katika maeneo yenye upungufu wa huduma za kijamii, umaskini wa kipato, kujengea uwezo jamii na taasisi za umma, kuunda vikundi vya uzalishaji.

TASAF AWAMU YA III 2013-

Halmashauri ya Arusha ni miongoni kati ya Halmashauri zinazotekelza Mpango wa TASAF awamu ya III kuanzia mwaka 2013 mpaka sasa na ni mpango wa miaka 10 mpaka mwaka 2023.

TASAF awamu ya tatu inalenga kuona miundombinu iliyowekwa katika awamu ya II inatoa huduma kwa mwanajamii kupitia kaya.

TASAF awamu ya tatu inatekeleza mradi wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini ambao unalenga kuwezesha kaya maskini sana kuongeza matumizi muhimu kwa njia endelevu.

Madhumini ya mpango ni kama ifuatavyo:-

- Kuwezesha kuwa na matumizi wakati wa hari.
- Kuwekeza katika rasilimali watu hususan watoto.
- Kuimarisha shughuli za kuongeza kiato.
- Kuongeza matumizi ya huduma za jamii.

Halmashauri ya Wilaya ya Arusha imeanza kutekeleza mpango wa TASAF awamu ya III kuanzia mwaka 2013 katika vijiji 45 katika kata 17 na mpango huu ulianza na jumla ya kaya 9,520.

ORODHA YA VIJIJI VILIVYOKO KWENYE MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI- HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

S/ N	KATA		VIJIJI	IDADI YA KAYA
1.	BANGATA	1.	BANGATA	129
		2.	MIDAWAWE	157
		3.	SASI	111
2.	BWAWANI	4.	BWAWANI	168
		5.	T/SIMBA	71
		6.	MUNGUSHI	65
3.	ILKIDING'A	7.	ILKIDING'A	430
		8.	ILKISONGO	588
		9.	OLOIGERUNO	537
4.	OLTUROTO	10.	KIVULUL	162
		11.	ILKIREVI	190
		12.	O' SAPUK	79
		13.	OLGILAI	187
5.	OLOIRIEN	14.	OLORIEN	238
		15.	SAITABAU(kwa sasa ni kata ya Tarakwa)	167
		16.	OLOSIVA	226
		17.	TARAKWA(kwa sasa ni kata ya Tarakwa)	107
6.	KIRANYI	18.	ILIKIUREI	136
		19.	KIRANYI	149
		20.	SIWANDET	143
7.	SAMBASHA	21.	SAMBASHA	145

		22.	SHIBORO	137
		23.	TIMBOLO	190
8.	KIMNYAKI	24.	KIMNYAK	82
		25.	OLEVOLOS	211
		26.	OLMRINGARINGA	195
9.	MOIVO	27.	MOIVO	285
		28.	OLTULELEI (kwa sasa ni kata ya Ilboru)	193
		29.	ILKILORIT	108
10.	SOKON II	30.	NG'IRESI	156
		31.	OLDADAI	122
		32.	SEKEI (kwa sasa ni kata ya Kiutu)	184
		33.	SOKONI II	145
11.	MWANDET	34.	IMBIBIA	304
		35.	LOSIKITO	218
12.	OLTRUMET	36.	ILKIUSHIN(kwa sasa ni kata ya Olmotony)	261
		37.	EKENYWA	555
13.	KISERIAN	38.	MLANGARINI	256
		39.	KISERIAN	160
14.	MATEVES	40.	LAROI	227
		41.	LEMUGUR	168
15.	OLMOTONY	42.	OLMOTONYI	150
		43.	NGARAMTONI	187
16.	KISONGO	44.	ENGORORA	223
17.	OLDONYOSAMBU	45.	OLDONYOWAS (kwa sasa ni kata Oldonyowass)	298
	JUMLA			9,200

Ili kufikia lengo awamu hii inatekelezwa katika sehemu kuu nne:-

1: MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI AMBAO UNATOA RUZUKU KWA KAYA MASKINI SANA HUSUSANI ZENYE WATOTO (UHAWILISHAJI FEDHA). PIA KUTOA AJIRA ZA MUDA KWA KAYA ZENYE WATU WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI.

a. Uhawilishaji fedha

Hii ni ruzuku inayotolewa kwa kaya zilizoko katika mpango kwa kipindi cha miezi miwili miwili. Ruzuku ziko za aina mbili:

i. Isiyo na masharti:

Ruzuku hii inatolewa kwa kaya zote ambazo ziko katika mpango kwa kiwango cha Tsh.20,000.

ii. Ruzuku ya masharti:

S/n	Kundi	Masharti	kiasi	Idadi ya watoto	Jumla ya ruzuku
1	Mtoto chini ya miaka 18 ambaye hayuko shuleni	Mtegemezi	4,000	1	4,000
2	Mtoto chini ya miaka 5	Kuhudhuria kliniki	4,000	1	4,000
3	Mtoto anayesoma shule ya msingi	Kuhudhuria shule siku	2,000	4	8,000

		zote			
4	Mtoto anayesoma kidato cha 1-4	Kuhudhuria shule siku zote	4,000	3	12,000

Awamu	Kipindi	Kiasi cha fedha Tsh.
i.	Julai/Agost,2015	427,680,000.00
ii.	Septemba/Oktoba,2015	394,937,250.00
iii.	Novemba/Desemba,2015	397,849,500.00
iv.	Januari/Februari,2016	398,925,000.00
v.	March/April,2016	352,164,750.00
vi.	Mei/Juni,2016	369,535,500.00
vii.	Julai/Agost,2016	355,292,250.00
viii.	Septemba/Oktoba,2016	372,073,500.00
ix.	Novemba/Desemba,2016	382,935,750.00
x.	Januari/Februari,2017	290,664,000.00
xi.	Mach/April,2017	294,816,300.00
	JUMLA	4,036,873,800.00

5	Mtoto anayesoma kidato cha 5-6	Kuhudhuria shuule siku zote	6,000	2	12,000
---	--------------------------------	--------------------------------	-------	---	--------

Endapo taarifa zitaonesha kuwa hawakuhudhuria ruzuku yao itaondolewa katika kipindi kinachofuata cha malipo.

Hadi kufikia April, 2017 jumla ya fedha Tsh. **4,036,873,800.00** zimeshatolewa kwa kaya maskini kama jedwali linavyoonesha:

Mwaka 2013 Mpango wa Kunifu Kaya Masikini ulianza na kaya 9,520 Hadi kufikia April,2017 zimebaki kaya 9,200. Upungufu huo unatokana na kutokuwa na sifa ya kuendelea kunufaika kwa sababu zifuatazo:-

- Muhusika wa kaya asiyekuwa na mtegemezi kufariki .
- Kaya kuhama bila kutoa taarifa.
- Zoezi la Uihakiki na kuondoa wanufaika wasiokuwa na sifa.
- Mfumo kuondoa wanufaika wasiojitokeza kuchuka/kupokea ruzuku yao kwa vipindi viwili mfululizo .

b. Ajira za muda

Hizi zinatolewa wakati wa utekelezaji wa miradi ya jamii yenye kulenga kutoa ajira ambapo walengwa hufanya kazi na kulipwa ujira kwa siku moja ni Tsh.2,300.00. 50% ya mradi inatumika kulipa walengwa na 50% inatumika kughramia mahitaji ya mradi (manunuzi na mafunzo).

2. KUONGEZA KIPATO CHA KAYA MASKINI KUPITIA UWEKAJI AKIBA NA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ILI KUBORESHA MAISHA (COMMUNITY SERVING AND INVESTMENT PROJECT-COMSIP).

i. Vikundi vya kuweke na kukopa

Hadi sasa jumla ya vikundi 66 vya kuweke na kukopa vya walengwa wa mpango vimeshaundwa katika vijiji 9.

Na.	Kijiji	Vikundi
1.	Bangata	6
2.	Midawe	9
3.	Ng'ires	8
4.	Oldadai	5
5.	Oltulelei	7
6.	Oldonyosapuk	5
7.	Olgilai	10
8.	Sasi	7
9.	Sokon II	6

ii. Miradi ya uzalishaji mali

Jumla ya miradi 4 ya uzalishaji mali imeibuliwa na inatekelezwa na walengwa wa mpango. Pia miradi mingine 6 imeibuliwa bado haijapitishwa TASAF makao makuu.

3. KUJENGA NA KUBORESHA MIOUNDOBINU INAYOLENGA SEKTA ZA ELIMU, AFYA NA MAJI

Jumla ya miradi 4 ya ujenzi wa miundombinu inatekelezwa. Pia miradi mingine 4 imeibuliwa bado haijapitishwa TASAF Makao makuu. Katika baadhi ya miradi hii ndipo wanufaika hupatiwa ajira za muda ili kuwaongezea kipato.

Miradi inayotekelezwa katika kujenga na kuboresha mioundombinu inayolenga sekta za Elimu, Afya na Maji ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali.

Lengo	Kijiji	Aina ya mradi	Thamani ya mradi- michango				
			TASAF Tsh.	Jamii Tsh.	H/mash auri Tsh	JUMLA Tsh.	
Kuongeza kipato cha kaya maskini kupitia shughuli za kiuchumi ili kuboresha maisha	1	Engorora	Ufugaji wa kuku chotara	21,782,090.00	6,417,000.00	0	28,199,090.00
	2	Ilkiushin	Ufugaji wa mbuzi wa maziwa	20,593,340.00	7,650,880.00	0	28,244,220.00
	3	Imbibia	Ufugaji wa mbuzi wa maziwa	20,593,340.00	7,650,880.00	0	28,244,220.00
	4	Losikito	Ufugaji wa mbuzi wa maziwa	20,593,340.00	7,650,880.00	0	28,244,220.00
Kujenga na kuboresha mioundombinu inayolenga sekta za elimu, afya na maji	5	Laroi	Ujenzi wa nyumba ya waalimu	71,760,886.00	7,522,000.00	5,507,000.00	84,789,886.00
	6	Themi ya Simba	Ujenzi wa madarasa 2, ofisi ya Mwalimu na matundu 6 ya chuo	71,760,886.00	7,522,000.00	5,507,000.00	84,789,886.00
	7	Bwawani	Ujenzi wa mfereji wa umwagiliaji (unatoa ajira ya muda)	74,656,000.00	344,000.00		75,000,000.00
	8	Lengur	Uhifadhi wa ardhi na udongo	70,545,814.00	0	0	70,545,814.00
	9	Kiserian	Uhifadhi wa ardhi na udongo (unatoa ajira ya muda)	70,545,814.00	0	0	70,545,814.00
JUMLA							

PICHA ZA MIRADI INAYOTEKELEZWA NA TASAF AWAMU YA III HALMASHAURI YA ARUSHA.

- 1. Picha za Wanufaika na Mpango wa Kususuru kaya Masikini ambao hupokea fedha za ruzuku kila baada ya miezi miwili katika vijiji 45 halmashauri ya Arusha.



2. Picha za Miradi ya Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya Mwalimu pamoja na ujenzi wa choo chenye matundu sita shule ya Msingi Themiyasimba kata ya Bwawani wenye thamani ya Tsh. 84,789,886.00 ikiwa Tsh. 71,760,886.00 fedha za TASAF, Tsh. 7,522,000.00 mchango wa Jamii na Tsh. 5,507,000.00 mchango wa Halmashauri.



3. Mradi wa Ujenzi wa nyumba ya waalimu yenye sehemu mbili (2 in 1) shule ya Msingi Laroi kata ya Laroi wenye thamani ya **Tsh. 84,789,886.00** ikiwa **Tsh. 71,760,886.00** fedha za TASAF, **Tsh. 7,522,000.00** mchango wa Jamii na **Tsh. 5,507,000.00** mchango wa Halmashauri.



4. Mradi wa Mazingira wa uhifadhi wa ardhi na udongo kijiji cha Kiserian kata ya Mlangarini, Mardi huu wanufaika wa Kaya masikini wanapata ajira ya muda kwa kufanyakazi ya kutunza mazingira na kulipwa ujira wa tsh. 2,300.00 kwa wiki. Mradi huu umegharimu kiasi cha Tsh. 70,545,814.00 fedha za mfuko wa TASAF.



5. Mradi wa Mazingira wa uhifadhi wa ardhi na udongo kijiji cha Lemugur kata ya Matevesi. Katika mradi huu wanufaika wa kaya masikini hujipatia ajira ya muda kwa kufanyakazi ya kutunza mazingira na kulipwa ujira wa Tsh. 2,300.00 kwa wiki. Mradi huu umegharimu kiasi cha Tsh. 70,545,814.00 fedha za mfuko wa TASAF.



6. Mradi wa Kuongeza kipato cha kaya maskini kupitia shughuli za kiuchumi ili kuboresha maisha katika kijiji cha Imbibia kata ya Mwandeti, Jumla ya Vikundi 10 vinafanya mradi wa ufugaji mbuzi wa Maziwa Mradi wenye thamani ya **Tsh. 28,244,220.00** Tsh. **20,593,340.00** fedha za zilizotolewa na **TASAF** na kiasi cha **Tsh. 7,650,880.00** fedha za mchango wa jamii.



7. Mradi wa Kuongeza kipato cha kaya maskini kupitia shughuli za kiuchumi ili kuboresha maisha katika kijiji cha Losikito kata ya Mwandeti, Jumla ya Vikundi 10 vinafanya mradi wa ufugaji mbuzi wa Maziwa Mradi wenye thamani ya **Tsh. 28,244,220.00** Tsh. **20,593,340.00** fedha za zilizotolewa na **TASAF** na kiasi cha **Tsh. 7,650,880.00** fedha za mchango wa jamii.



-Miradi iliyoibuliwa

na	Kijiji	Aina ya Mradi ulioibuliwa
1.	Oldonyowass	Ufugaji wa kuku chotara
2.	Olmotony	Ufugaji mbuzi wa maziwa
3.	Olgilai	Ufugaji mbuzi wa maziwa
4.	Shiboro	Ufugaji mbuzi wa maziwa
5.	Oldonyosapuk	Ufugaji wa mbuzi wa maziwa
6.	Ng'ires	Ufugaji mbuzi wa maziwa
7.	Midawe	Ujenzi wa zahanati
8.	Samabasha	Ujenzi wa madarasa 2, ofisi ya mwalimu na choo matundu sita
9.	Mungushi	Ujenzi wa nyumba 1 ya waalimu(two in one)
10.	Timbolo	Ujenzi wa mifereji ya umwagiiaji

4. KUJENGA UWEZO KATIKA NGAZI ZOTE ZA UTEKELEZAJI.

Utekelezaji wa mpango huanzia ngazi ya Taifa hadi kijiji. Katika ngazi hizi mafunzo na miongozo imekuwa ikitolewa kila wakati inapohitajika ili kuboresha utendaji wa kazi. Wahusika ni timu za uwezeshaji, katika ngazi ya Halmashauri kuna timu ya wawezeshaji yenye wataalam 22 kutoka katika sekta mbalimbali inaosimamiwa na Mratibu wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Katika ngazi ya kijiji kuna kamati ya mpango yenye wajumbe 14 wanaotokana na wananchi inayosimamiwa na Mwenyekiti wa kijiji na Afisa Mtendaji wa Kijiji.

Kutokana na Changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa Miradi ya TASAF kama:-

- Vitambulisho vya mpango kutokuwa na picha ya mlengwa wakati wa malipo inachukua muda mrefu kuhakiki nyaraka ili kudhibitisha mlengwa.
- Walengwa kupoteza vitambulisho vya mpango.
- Kuongezeka wa idadi ya wahitaji ambapo hakuna maelekezo ya kuweza kuongeza idadi ya walengwa kwa sasa.
- Wananchi kutoa taarifa za uongo na kupelekeza baadhi ya watu wasio na sifa kuingizwa kwenye mpango.
- Kupewa miradi michache kutoka TASAF Makao makuu ilikinganishwa na mahitaji makubwa ya jamii.
- Mpango hauna kipengele maalum kinacholenga watu wenye mahitaji ya tofauti kama vile wazee, walemavu.
- Mabadiliko ya mipaka ya maeneo kwa kuanzishwa kwa kata mpya, vijiji vipya na vitongoji vipya vilivyokuwa vijiji zamani, wakati mpango unatekelezwa kwa kufuata mipaka ya zamani

Kitengo cha TASAF kimejipanga kukabiliana na Changamoto hizo kwa kuwa na mikakati ifuatayo:-

- Kuendelea kufanya uhakiki wa walengwa walioko kwenye mpango wa nyumba kwa nyumba ili kubaini kama wana vigezo.
- Kuwasiliana na TASAF Makao makuu ili waone jinsi ya kuweza kuweka picha katika vitambulisho vya walengwa.
- Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kujenga uelewa wa mpango na jinsi unavyotekelezwa.